TANGAZO LA SERIKALI NA. 283 la tarehe 7/4/2023

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 107)*

NOTISI YA MSAMAHA WA KUSAFIRISHA MAGOGO YA MTI AINA YA MKURUNGU NJE YA NCHI YA MWAKA 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Msamaha wa Kusafirisha Magogo ya Mti Aina ya Mkurungu Nje ya Nchi ya Mwaka 2023.

Msamaha wa kusafirisha magogo

2.-(1) Kampuni ya *Dazhong Wood Industry Company Limited* inapewa msamaha wa kusafirisha magogo ya mti aina ya mkurungu unaojulikana kwa jina la kisayansi kama *Pterocarpus Tinctorius* kwenda nchini China pasipo kuchakatwa.

(2) Kiwango cha magogo yaliyoruhusiwa kusafirishwa nje ya nchi na Kampuni iliyotajwa katika aya ndogo ya (1) kitakuwa kama kilivyoainishwa katika aya ya 4.

Umuhimu na sababu za kutolewa kwa msamaha

3. Msamaha huu unatolewa kutokana na umuhimu na sababu zifuatazo:

(a) magogo ya mkurungu yanayopewa msamaha wa kusafirishwa kwenda nje ya nchi bila kuchakatwa yamepinda na hayawezi kuchakatwa kirahisi na kusagwa katika viwanda vya mbao ndani ya nchi;

(b) kukuza masoko ya magogo ya mti aina ya mkurungu kwa kuwa masoko ya magogo haya yanapatikana nchini China na Kampuni ya

*Dazhong Wood Industry Company Limited* imeahidi kusaidia upatikanaji wa masoko zaidi ya mazao ya misitu yanayopatikana hapa nchini; na

(c) Kampuni ya *Dazhong Wood Industry Company Limited* imeonyesha kwamba upo usimamizi endelevu wa magogo ya mkurungu na itahakikisha kwamba inatoa mchango kwa viwanda vya kuchakata mbao ndani ya nchi.

Masharti ya msamaha

4. Msamaha huu unatolewa kwa masharti yafuatayo:

(a) kiwango cha magogo ya mti wa aina iliyotajwa katika Notisi hii kitakuwa ni magogo 8,950 yenye mita za ujazo 656.219; na

(b) aina hii ya magogo na kwa kiwango tajwa itasafirishwa kwenda nchini China.

Muda wa msamaha

5. Msamaha huu utatumika kwa kipindi cha siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii.

Dodoma,
23 Machi, 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*